## 07- Matayarisho Kabla Ya Hajj

Safari ya Hajj inahitaji matayarisho kama vile inavyohitajika katika safari zozote nyinginezo. Ila safari hii inahitaji zaidi ikhlaasw, taqwa na subira ya hali ya juu. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ ٱلۡحَجُّ أَشۡهُرٞ مَّعۡلُومَٰتٞۚ فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلۡحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي ٱلۡحَجِّۗ وَمَا تَفۡعَلُواْ مِنۡ خَيۡرٖ يَعۡلَمۡهُ ٱللَّهُۗ وَتَزَوَّدُواْ فَإِنَّ خَيۡرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقۡوَىٰۖ وَٱتَّقُونِ يَٰٓأُوْلِي ٱلۡأَلۡبَٰبِ ١٩٧

**((Hajj ni miezi maalumu. Na atakayekusudia kuhiji (akahirimia), basi asifanye tendo la ndoa wala ufasiki wala mabishano katika Hajj. Na lolote mlifanyalo katika ya kheri Allaah Analijua. Na chukueni masurufu. Na hakika bora ya masurufu ni taqwa. Na nicheni Mimi enyi wenye akili!))[1]**

Kwa hiyo jiandae vizuri kwa yafuatayo ili safari yako na 'ibaadah zako zote ziwe sahali na kamilifu In Shaa Allaah.

### *1*-Niyyah

Kwanza kabisa weka niyyah moyoni mapema kabla ya lolote kwa ajili ya kutekeleza 'ibaadah hii kwamba unaitekeleza kutimiza maamrisho ya Allaah (سبحانه وتعالى) na Rasuli Wake (صلى الله عليه وآله وسلم) na isiwe niyyah yako kwa lengo la manufaa ya kidunia au kujionyesha kwa watu. Muombe Allaah (سبحانه وتعالى) Ajaalie iwe yenye kumridhisha Yeye Pekee ili Akulipe malipo mema kama Alivyotuahidi.

### 2-Du'aa

Baada ya niyyah, omba du'aa kwa wingi Allaah (سبحانه وتعالى) Akuruzuku *Tawfiyq* ya kuifanikisha safari hiyo na uweze kukamilisha fardhi hii kwa sahali na ukamilifu na Akutakabalie juu ya kuweko mapungufu katika 'ibaadah

[1] Al-Baqarah (2: 197).

zako. Pia muombe Allaah (سبحانه وتعالى) Akurudishe nyumbani kwa salama na amani.

**3-Matayarisho Ya Usafiri**

Kawaida mahitajio yote ya safari na huduma safarini zinaandaliwa na shirika linalopeleka Mahujaji. Kila nchi ina kanuni zake za utoaji viza. Unahitajika kuwa na pasipoti isiyokuwa inamalizika muda wake chini ya miezi sita. Maandalizi yote; viza, tiketi, makazi ya huko, usafiri, matembezi n.k. yanashughulikiwa na shirika unalojiunga nalo. Ulizia mashirika kadhaa upate kujua huduma zao na gharama zake kisha ulinganishe na uchague iliyokuwa munaasib kwako. La **muhimu kabisa** ni kuchagua shirika linalotoa mafunzo kutokana na Qur-aan na Sunnah na Manhaj ya *Salafus-Swaalih* ili uweze kutekeleza Hajj yako kama alivyoamrisha Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ***((Chukueni manaasik zenu (za Hajj) kutoka kwangu))***.

Utakapokwisha jiunga na shirika la kuhudumia Mahujaji, utaanza kujiandaa kwa yafuatayo:

**4-Deni**

Lipa madeni yako yote. Unaweza kutekeleza Hajj ikiwa unalo deni ambalo litawezekana kulipwa wakati haupo, mfano kulipwa kwako mshahara unaopokea kila mwezi. Andika *wasiyyah* kwa watu wako kuhusu deni lolote ambalo unaliacha nyuma yako na ambalo litaweza kulipwa kutokana na mali utakayoiacha pindi ukiaga dunia safarini. Ikiwa ni deni ambalo huna uwezo nalo kulilipia nyuma yako, basi haikupasi kutekeleza Hajj kwanza mpaka ulipe deni la watu. Kutokulipa deni ni jambo la hatari linaloweza kumzuia mtu kuingia katika Jannah. Kwa hiyo hakikisha umelipa madeni yote au umeandaa lilipwe.

***5-Waswiyyah***

Andika *wasiyyah* wako kama inavyokubalika kishariy'ah. Muislamu inampasa aandike *wasiyyah* wake na kurekebisha lolote kila baada ya siku tatu. Basi anayekwenda Hajj anawajibika zaidi kuandika *wasiyyah* kwani huenda ikawa ndio majaaliwa yake ya kuaga dunia huko.

## 6-Kuaga Watu Na Kuomba Msamaha[2]

Adabu za Kiislamu katika mas-ala ya safari zinafundisha kuagana na kuombeana du'aa zilizothibiti katika Sunnah. Pia ni vizuri kuomba msamaha kwa ndugu akiwa wa damu au udugu wa Kiislamu ambaye umekhasimikiana naye. Mwanachuoni Ibn Baaz (رحمه الله) amesema katika Fataawa za Hajj Mlango wa: '***Adaab As-Safar lil-Hajj*** (baada ya kutaja kukimbilia kuomba tawbah ya kweli kutokana na kila dhambi) **"…**juu ya hivyo ikiwa madhambi hayo yanahusiana na kuwatendea ubaya watu; kuua, kuiba, kumtukana mtu, basi watu hao (waliomkosea ndugu yao) warudishe walichochukua kwa dhulma au waombe msamaha kwa ambao wamewakosa kabla ya kusafiri". Pia Hadiyth zifuatazo zimekemea vikali kuhusu kukhasimikiana kwamba amali za Muislamu hazipokelewi pindi kukiweko na uhasama kati yake na nduguye Muislamu.

Hadiyth ya Abu Huraryah (رضي الله عنه) kwamba Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

**((تُعْرَضُ الْأَعْمَالُ فِي كُلِّ يَوْمِ خَمِيسٍ وَاثْنَيْنِ فَيَغْفِرُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ فِي ذَلِكَ الْيَوْمِ لِكُلِّ امْرِئٍ لَا يُشْرِكُ بِاللَّهِ شَيْئًا إِلَّا امْرَأً كَانَتْ بَيْنَهُ وَبَيْنَ أَخِيهِ شَحْنَاءُ فَيُقَالُ ارْكُوا هَذَيْنِ حَتَّى يَصْطَلِحَا ارْكُوا هَذَيْنِ حَتَّى يَصْطَلِحَا))**

***(('amali njema hutandazwa kila Alkhamiys na Jumatatu, kisha Allaah Aliyetukuka Humghufuria kila mtu asiyemshirikisha na kitu Allaah, isipokuwa mtu aliyekuwa baina yake na baina ya ndugu yake uhasama, Husema: Waacheni hawa wawili mpaka wapatane; Waacheni hawa wawili mpaka wapatane))***[3]

Juu ya hivyo, safari ya Hajj ni safari ya kutegemea mtu kufutiwa madhambi yote, kwa hiyo inapasa kwanza ujisafishe na dhambi khasa zinazohusiana na dhulma za watu. Pia hakuna uhakika wa kurudi nyumbani kwani huenda kifo kikakukuta huko safarini. Kwa hiyo imuingie khofu kila mmoja wetu kwamba pindi mtu akiaga dunia hali ya kuwa amekhasimiana na mwenziwe hatoingia katika Jannah kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

[2] Rejea Hiswnul-Muslim na Hiswnul-Mu-umin kupata du'aa za kuaga watu.
[3] Muslim.

**((لا يَحِلُّ لِمُسْلِمٍ أَنْ يَهْجُرَ أَخَاهُ فَوْقَ ثَلاَثِ لَيَالٍ، يَلْتَقِيَانِ فَيُعْرِضُ هَذَا وَيُعْرِضُ هَذَا، وَخَيْرُهُمَا الَّذِي يَبْدَأُ بِالسَّلامِ))** رواه البخاري ومسلم وَ في رواية أبو داود بإسناد على شرط البخاري ومسلم:

**((فَمَنْ هَجَرَ فَوْقَ ثَلاَثٍ فَمَاتَ دَخَلَ النَارَ))**

***((Haimpasi Muislamu amhame ndugu yake zaidi ya siku tatu hata wanapokutana huyu anamgeuzia (uso) huyu na huyu anamgeuzia (uso) huyu. Na aliye mbora wao ni yule anayeanza kutoa salaam))***[4]

***((Atakayemhama (mwenzake) zaidi ya siku tatu akafariki basi ataingia Motoni))***[5]

**7-Pesa za matumizi**

Kawaida muongozo hutolewa na shirika utakalojiunga nalo, lakini huenda haya yakakusaidia:

- Badilisha pesa kiasi za kuanzia matumizi huko, nyinginezo badilisha katika hundi ya wasafiri ('traveller's cheque') au tumia kadi za benki maarufu ambazo utaweza kutoa kila unapohitaji huko. Shirika unalokwenda nalo watakuarifu masiku mangapi jumla ya safari, hivyo utaweza kujipangia kiasi cha pesa za kuchukua kutokana na haja na uwezo wako. Utahitaji nakala ya pasipoti kwa ajili ya benki kukubadilishia pesa zako kwa hiyo andaa kuchukua nakala kadhaa za vitambulisho vyako.

- Fanya nakala ziada za kila kitu; pasipoti, vitambulisho, hundi ya wasafiri n.k.

- Vizuri ukiwa na uwezo kuchukua pesa ziada kwa ajili ya kutolea swadaqah huko kwani malipo yake ni maradufu.

- Andika namba za cheki zote katika kijitabu kidogo na thamani zake. Pia fanya nakala ya kila moja uweke akiba pindi za asili zikipotea

[4] Al-Bukhaariy na Muslim.
[5] Abu Daawuwd kwa isnaad yenye sharti ya Bukhaariy na Muslim.

- Weka pesa zako katika kipochi kilicho madhubuti na usitembee na pesa zako zote nje ya hoteli kwani inasikitisha kutanabahisha kwamba kuna wezi ambao hata wakati wa kutufu *Al-Ka'bah* wanaibia watu! Unapoweka pesa zako katika begi lako, usiweke katika sehemu husika, bali weka sehemu asiyotegemea mwizi; mfano katika mfuko wa nguo zako begini, au kipaketi cha dawa meno n.k.

- Unapoweka pesa zako hotelini katika begi lako, hakikisha umelifunga vizuri na ufunguo unauhifadhi vizuri mwenyewe katika mkanda utakaouvaa kiunoni (wanaume). Ama wanawake, shonea nguo yako ya ndani kifuko cha zipu uweze kuhifadhi humo funguo zako.

**8-Jifunze Fiqh Ya Hajj**

Jifunze Fiqh ya Hajj ili uweze kujiandaa vizuri utekelezaji wa 'ibaadah hii tukufu ambayo inahitaji ufanisi wa 'amali ili usipoteze muda na mali yako bure kwa kuiharibu pindi ukiitekeleza ndivyo sivyo. La kuzingatia zaidi ni kujiepusha na kila jambo lisilothibiti katika mafunzo ya Qur-aan na Sunnah na hakikisha mafunzo yote unayoyapata ni mafunzo swahiyh yasiyo na shaka. Mashirika ya Hajj, kawaida huwa yanatoa mafunzo kabla ya safari.

**9-Hifadhi Du'aa Za Manaasik**

Rejea mlango wake katika kitabu hiki ujitahidi kuzihifadhi du'aa hizo ili iwe wepesi kabisa kwako kutekeleza 'Umrah na Hajj yako kwa sababu kutokana na zahma kubwa, inakuwa vigumu mtu kutazama kitabu kuzisoma hizo du'aa; na vitabu vingi vya du'aa vinavyouzwa huko, havina mashiko; du'aa zake hazijathibiti, bali ni taklifa. Ukiweza kuzihifadhi hizo du'aa chache zilizothibiti, itakuwa sahali mno kwako na utaweza kutimiza kikamilifu Hajj yako.

**10-Chunguza Magonjwa Na Chanjo**

Ni vyema kufanya vipimo hospitalini kabla ya kuondoka ili kuhakikisha huna magonjwa yoyote ambayo huenda yakachomoza huko safarini yakakuzuia kutekeleza 'ibaadah yako.

Pia piga chanjo zote zinazohitajika uchukue vyeti vyake. Bila shaka utafahamishwa hili na shirika unalojiunga nalo.

## 11-Begi

- Jaribu kununua begi lisilokuwa zito wala kubwa mno kwani kuna taabu yake katika usafiri na pia dhiki ya sehemu ya kuliweka hotelini kwani vyumba huko si vyenye nafasi kubwa ya kutosheleza mizigo mikubwa. Kumbuka pia kwamba zawadi kubwa watu wanayopenda kuchukua kurudi nayo ni maji ya Zamzam ambayo hayatoingia katika begi bali utahijtaji kuyabeba pekee.

- Chukua pia kibegi kidogo cha kitambaa na zipu, au kibegi cha mgongoni, kutumia wakati utakapoelekea *Minaa* kwa masiku hadi umalize taratibu za huko; yaani kuanzia tarehe 8 Dhul-Hijjah hadi tarehe 12 au 13 Dhul-Hijjah.

- Baada ya kufunga begi lako, weka alama kama ribini au kitambaa cha rangi kwenye mkono wa begi, au andika jina lako ili uweze haraka kulitambua begi lako unaposubiri mabegi kuteremeshwa kutoka katika ndege.

## 12-Vitu Utakavyohitaji Kuchukua

Aghlabu ya vitu vinapatikana kwa usahali Makkah na Madiynah, lakini tunavitaja hapa pamoja na maelezo ziada ya kutanabahisha. Kwa hiyo orodha hii ya vitu unaweza kununua huko huko Makkah au Madiynah. Kwa hiyo mtu atapima mwenyewe kama atapendelea kununua hivi vitu mapema nchini mwake au atapenda kununua huko, lakini ni bora kununua kabla ya safari ili ujifanyie wepesi kwani uendako ni ugenini na utaweza kuhifadhi muda wako kwa 'ibaadah badala ya kwenda madukani.

Kwa wale ambao watahirimia katika ndege kwa ajii ya kufanya 'Umrah, hutohitaji vitu vya kufanya ghuslu kwa sababu utahitajika kufanya ghuslu tokea nyumbani kwako. Ama wanaofikia Madiynah kwanza, hao

watahitaji kuwa na vitu vyao tayari kwa sababu watahirimia katika Miyqaat ambako atahitajika kufanya ghuslu (kuoga josho).

| Mahitaji ya Msalani (Chooni) | |
|---|---|
| **Cha kuchukua** | **Tanbihi** |
| Shampuu | Wanawake zaidi wanahitaji lakini zisiwe zenye manukato. |
| Karatasi za tisshu | Vipaketi vidogo dogo ambavyo vinaingia katika kibegi cha mkononi cha mwanamke. Hakikisha usinunue zenye manukato. |
| Sabuni ya maji ya kuogea | Inakuwa sahali kuitumia safarini khasa utakapokuwa *Minaa*. Pia ni afya zaidi kutumia kuliko sabuni ya kawaida. Hakikisha kuwa haina manukato. |
| Sabuni ya maji ya mkono iwe ya kuua viini, vidudu. | Ni sahali kutumia na kusafiri nayo na ni afya zaidi kuitumia. |
| Waipa za karatasi za kuua viini vidudu | Daima weka katika kibegi cha mkononi kutumia khasa kabla ya kutawadha au kula chakula kwani si wepesi kupata maji ya kunawaia mkono. Utazihitaji msalani pia. |
| Dawa ya mswaki | Miswaak ya Sunnah pia inapatikana tele huko na vizuri kuitumia kila mara. |
| Dawa ya kusukutilia mdomo au karafuu, hiliki. | Ni vyema kuwa na dawa ya kusukutilia mdomo kuhifadhi harufu ya mdomo khasa asubuhi unapoamka na kwenda Masjid. Tahadhari! Aghlabu ya dawa hizi zina alkoholi lakini ziko pia zisizo na alkoholi, kwa hivyo hakikisha au chukua karafuu na hiliki |

| | |
|---|---|
| | katika kichupa kidogo, uwe unazitafuna na kuzisukutulia baada ya kupiga mswaki kwani zinakata vizuri harufu mbaya ya mdomo. Tambua kwamba kuna Hadiyth ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliyotamani kuamrisha Muislamu apige mswaki kabla ya kila Swalaah! Na tambua pia kwamba Malaika wanaridhika na harufu nzuri na wanaudhika na harufu mbaya! |
| Diodorani - dawa ya kwapani | Isiwe yenye manukato. Au tumia shabu ambayo haina harufu na unaweza kuichanganya na podari isiyokuwa na manukato. |
| Pedi na vibandiko vya chupi. | Wanawake watahitaji ili kujihifadhi pindi imewatokezea hedhi. Vibandiko vya chupi vinasaidia mno kubakisha chupi ya mwanamke safi na kujipunguzia mashaka ya kuzifua kwani hizo huwa unabadilisha tu pindi ikichafuka na chupi inabakia kuwa safi kwa muda wa siku nzima. Hii itakusaidia sana katika Ihraam kwani pindi chupi ikichafuka si wepesi kupata kuifua msalani hadi urudi hotelini.<br><br>Weka chache katika handbag yako kila mara uwe nazo akiba. |

| **Mahitaji Ya Ihraam** | |
|---|---|
| **Cha kuchukua** | **Tanbihi** |
| Wanaume - shuka za Ihraam na mkanda wa kujifunga kiunoni wenye sehemu ya kuhifadhi pesa. | Zinapatikana kwa urahisi madukani katika nchi unayotoka. Ni vyema kununua jozi mbili ya nguo za Ihraam kwani utabakia katika Ihraam siku 3 takriban kuanzia tarehe 8 Dhul-Hijjah. |

| | |
|---|---|
| Makubadhi | Viatu vya ngozi – vinapatikana maduka ya nguo za Ihraam. |
| Vifaa vya kunyolea nywele na sehemu za siri – vya kutumia na kutupa. | Ikiwa umekosa kinyozi wakati wa kujivua Ihraam. Na pia kujisafisha nywele sehemu za siri khasa siku ya tarehe 10 Dhul-Hijjah.<br><br>Tanabahi: Ihraam ya mwanzo kwa ajili ya 'Umrah ni vizuri kujisafisha ukiwa bado uko kwako ili usipate tabu tena utakapofika *Miyqaat* ikiwa unatokea Madiynah. Ama wanaotanguliza 'Umrah moja kwa moja baada ya kufika mjini Jeddah, wao wanapaswa wawe wameshaingia Ihraam katika ndege na hivyo watakuwa wameshaoga majumbani mwao. |
| Mkoba mdogo | Wa mkanda unaovaliwa shingoni na kubakia mbele yako unapotembea kuhifadhi pesa na vitu vidogo muhimu; simu, kadi za benki n.k. |
| Nguo na mahitaji ya wanawake katika Ihraam na nje ya Ihraam | Nguo zozote zinafaa ila ziwe zimetimiza masharti ya hijaab[6]. Si lazima kuvaa nguo nyeupe au ya kijani wala si katika Sunnah bali mwanamke anaweza kuvaa nguo zake zozote zile. Chukua nguo nyepesi zilizo wepesi kuzifua na zisizohitaji kupigwa pasi. Utahitaji kubadilisha nguo ukiwa katika Ihraam kwa muda wa siku nne takriban.<br><br>Wanawake washoneshe mifuko ndani ya nguo zao za ndani ili wahifadhi pesa zao. Juu yake wavae 'abaayah. |
| Baibui/'abaayah | Kiasi matatu. Ukiwa katika Ihraam *Minaa*, utahitaji angalau mawili kwani ni wepesi |

[6] Tazama mlango unaohusu Wanawake.

| | |
|---|---|
| | kuchafuka. 'Abaayah zisiwe za kuonyesha mwili, na zisizo na marembo wala rangi, yawe pleni kabisa bila ya urembo wowote ule bali ziwe pana zisizobana mwili, zisizo na uwazi wowote, bali zenye kufunika nguo nzima na mwili mzima mpaka miguuni. |
| Khimaar au mtandio | Utahitaji Khimaar au mitandio mirefu na mipana ya kukufunika tokea kichwani hadi angalau magotini ili ubakie katika sitara ya hijaab inayopasa kishariy'ah.<br><br>**MUHIMU:** Mwanamke haimpasi kufunika uso wake na kuvaa glavu katika Ihraam ila inapokuwa kuna wanaume akachelea fitnah, kwa hali hiyo atatakiwa kujifunika uso wake lakini si kwa niqaab au burqah bali kwa ghashwah au kitambaa chepesi kisichobana uso.[7] |
| Suruwali ndefu za kuvalia ndani badala ya gaguro. | Kwa ajili ya kujisitiri. Hizi ni vyema kuzitumia kila mahali kwani ni sitara kubwa kwa mwanamke pindi unapopanda na kushuka gari ujisitiri miguu yako isionekane. Pia inapotokea ajali (Allaah Atuhifadhi), unasitirika kwa kutokukashifu mwili wako na sehemu za siri. Katika Ihraam ndio kuna umuhimu mkubwa wa kuzivaa. |
| Soksi. | Ufunike miguu yako wakati wote mpaka katika Swalaah. Chukua jozi kadhaa kwani ni wepesi kuchafuka, utahitaji kubadilisha mara kwa mara. Soksi zitakusaidia pia kufanya *Mas-hul-Kufayn*[8] . |

[7] Tazama mlango unaohusu Wanawake katika nukta ya 'Ihraam'
[8] Kufanya wudhuu juu ya soksi.

| | |
|---|---|
| Mkoba mdogo wa mkanda mrefu | Utahitaji mkoba mdogo wa kutumia wakati unapofanya *Twawaaf* na *As-Sa'-y* kwani kubeba mkoba mkubwa unachosha. Mkoba mdogo wenye mkanda unaoweza kuuvaa begani kwa upande ili mkoba uwe mbele yako unapouvaa kwa ajili ya kujilinda na kuibiwa pesa na wachomoaji. Humu unaweza kujitilia vitu vyako vya muhimu kabisa kiasi cha muda huo wa kutekeleza *Twawaaf, As-Sa'-y* n.k. |
| Taulo | Ya kiasi kujifutia maji, nyepesi na nyinginezo ndogo ndogo. Ni vizuri kutumia taulo ndogo kulikoni kubwa kwa sababu ya usahali wa kufua na kuanika ikiwa unafikia hoteli zisizotowa huduma za vitu kama hivyo. |
| Sabuni ya kuogea. | Mahujaji watumie sabuni zisizokuwa na manukato. |
| Viatu | Wanawake viatu vyovyote ambavyo vinaweza kutumika kufanyia wudhuu na kuingia navyo msalani. Pia viwe vyepesi kuvibeba na kuingia navyo Msikitini unapiviweka katika mifuko. |
| Mfuko mdogo wa kitambaa au plastiki | Kwa ajili ya kutilia viatu vyako unapoingia Masjid hasa kwa ajili ya Masjid An-Nabawiy kwani mifuko ya bure inapatikana Masjid Al-Haraam unapoingia tu ndani ya Msikiti. |
| Mkasi mdogo | Wanawake kwa ajili ya kukata nywele zao kidogo kujitoa katika Ihraam. Usipeki mkasi katika mkoba wa mkononi kwani hairuhusiwi kuingia nao katika ndege. |

| Nguo Za Kawaida | |
|---|---|
| **Cha Kuchukua** | **Tanbihi** |
| Kanzu, fulana, shuka au suruwali ya kuvalia ndani ya kanzu | Wanaume: Haifai kuchukua fulana au mashati yenye picha, nembo n.k.<br><br>Tanbihi kwa wanaume na wanawake: Huduma za udobi zimejaa barabarani huko kwa hiyo usijibebeshe nguo nyingi. |
| Nguo za ndani, niqaab, skafu za hijaab, mitandio (shela), kanga mbili tatu n.k. | Mwanamke atahitaji kubadilisha nguo za ndani mara kwa mara, kwa hiyo chukua za kukutosheleza. Kanga na mitandio ya pamba utahitaji kujifunikia hotelini ingawa si muda mrefu utakaokuwa unashinda humo.<br><br>**MUHIMU!** Kina dada jifunikeni nyuso zenu kwa niqaab au ghashwah (mtandio unaoufunika uso), kuepukana fitnah za wanaume na fitnah za video na wahalifu wanaorekodi huko kila sehemu! |
| Nguo za kulalia | Wanaume kanzu nyepesi au fulana na msuri (kikoi).<br>Wanawake nguo za nyepesi za pamba. |

| Misahafu, Vitabu | |
|---|---|
| **Cha Kuchukua** | **Tanbihi** |
| Mus-haf (Qur-aan) | Mdogo utakaoweza kuuweka katika mkoba wako kila mahali kwani wakati mwengine si wepesi kuipata Misahafu |

| | |
|---|---|
| Msahafu wa Tarjama mdogo. | iliyoko Masjid. Unaweza kuifuatilia lakini utakaporudi utakuta mahali pako pameshakaliwa!<br><br>Ni vizuri Muislamu kutumia muda wake wa faragha kusoma na kufahamu maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى). Utakapokuwa *Minaa* chukua fursa hii kusoma Tarjama ya Qur-aan. |
| Miwani ya kusomea | Kwa wenye udhaifu wa macho khasa ikiwa utachukua msahafu mdogo.<br>Ni vyema kuchukua moja ziada kama akiba pindi ikipotea moja. |
| Kitabu cha du'aa | Hiswnul-Muumin au Hiswnul-Muslim ambacho kina adhkaar za asubuhi na jioni pamoja na du'aa mbali mbali anazozihitaji Muislamu katika maisha yake kila siku. Ni vyema kuzihifadhi khasa zile za Swalaah ili uweze kutekeleza Swalaah zako kikamilifu na kwa uzuri kabisa.<br><br>Ukitaka kuchukua vitabu vinginevyo vya du'aa na adhkaar, hakikisha unachukua vilivyothibiti katika Sunnah, usije ukapoteza muda wako na juhudi kwa 'amali zisizokubaliwa. Rejea mlango wa 19 mlango wa du'aa za Sunnah ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) katika kitabu hiki zimeandaliwa ambazo zinamtosheleza Muislamu kuzisoma. |
| Kitabu cha Fiqh ya Hajj | Kinapatikana maduka ya vitabu, na pia hiki kitakutosheleza.<br><br>Ukiwa na swali ambalo hukulipata mwelekezo, kuna huduma za Fataawa |

| | |
|---|---|
| | katika *Masjid Al-Haraam*. Kila mahali zimewekwa simu ukinyanyua tu anapokea mtu kukujibu swali lako. Au pia uliza wahusika uliojiunga nao. Ni vyema kuuliza jambo kuliko kuona haya kuuliza ukafanya makosa. |

| **Mahitaji Mengineyo** | |
|---|---|
| **Cha Kuchukua** | **Tanbihi** |
| Viatu vya raba vya mazoezi. | Pia ni vizuri kuwa na jozi ya viatu vya aina hii kwa ajili ya kuvitumia utakapokuwa *Minaa* kwa vile utakuwa na mwendo wa panda shuka huku na kule kuliko kuvaa ndara au makubadhi. |
| Kifuko kidogo mno cha plastiki au kitambaa (viwe vitatu) | Kutilia vijiwe vya *Jamaraat* ukihofia kuvipoteza baada ya kuviokota. |
| Mkoba au mfuko | Wa kuweza kuchukua Masjid na kila mahali na kutia vitu vyako muhimu kama Msahafu, dawa, miwani, mswala mwepesi, karatasi za tisshu, pesa za matumizi kidogo, n.k. |
| Pochi ya pesa | Inayokufaa. |
| Mswala wa kujikunja au midogodogo ya kuingia katika mkoba mdogo | Kwa ajili ya kuuchukua kila uendapo safarini kwani huenda ukakosa mahali ndani ya Masjid au baadhi ya Misikiti ya njiani haina mazulia masafi. Pia unaweza kuutumia kulalia utakapokesha *Muzdalifah*. |

| | |
|---|---|
| Kalamu na kitabu kidogo. | Cha kuandikia maelezo na orodha ya kujikumbusha. |
| Simu ya mkono. | Kwa ajili ya mawasiliano ya dharura. Kadi za simu zinapatikana Saudia na zimejaa kila mahali kwa bei nafuu kabisa.<br><br>**Lakini Hakikisha unazima simu yako kila unapokuwa Msikitini**!<br><br>Ni busara kila mmoja; mume na mke awe na simu yake kwani huenda mkahitaji kuwasiliana baada ya kutoka Masjid na khasa ikitokea mmepoteana. |
| Chaji ya simu na adapta (kirekebishi) | Hakikisha chaji inafanya kazi na ukiweza kuchukua moja ziada ni vizuri. Adapta ni muhimu kabisa uweze kuchaji simu yako kwani baadhi ya hoteli hawaweki. |
| Kufuli ya begi | Tengeneza ufunguo mwengine ikiwezekana ili ukipotea mmoja uwe na wa pili. |
| Begi dogo la kubeba mgongoni. | Utalihitaji wakati wa safari ndogo kama kwenda baina ya *'Arafah*, *Muzdalifah*, Makkah na *Minaa*. |
| Kikatio kucha | Kwa kukata kucha zako kabla hujahirimia, na baada ya kumaliza Hajj. |
| Kitana, brashi | Chukua ndogo ndogo tu. |
| Saa ya kengele ikiwa hutumii ya simu. | Ikuamshe nyakati za 'ibaadah. Aghlabu simu za mkono zinazo huduma hii. |

| | |
|---|---|
| Chupa ndogo ya maji ya kunywa. | Utaweza kujitilia maji ya zamzam ukipenda kila unapotoka Masjid. Utahitaji haya khasa siku za joto lakini maji ya kuuzwa chupani yanapatikana kwa sahali huko. |

| **Visivyopasa Kuchukua** | |
|---|---|
| **Kisichopasa Kuchukua** | **Tanbihi** |
| Kamera pamoja na video kamera, n.k. Hata simu zenye kamera. | Hairuhusiwi kwani huko ni sehemu ya kutekeleza 'Ibaadah na haendi mtu kwa ajili ya matembezi au utalii. Jambo hili linapaswa kukatazwa mno kwani imekuwa ni fitnah kubwa siku hizi kurekodi hata katika kutufu *Al-Ka'bah*, *As-Sa'-y* na kwengineko. Na simu zote za mkono siku hizi zina kamera, na kupiga au kupigwa picha zisizo za dharura ni haraam! kwa hiyo **TAHADHARI** na kuingia katika fitnah hii usiharibu Hajj yako. |
| Mapambo ya thamani; dhahabu, saa za ghali n.k. | Mwanamke hatakiwi kujipamba kabisa kwa mapambo yoyote yale. |
| Visu, aina zozote za silaha, vitu vya maji. | Hairuhusiwi kubeba hivi katika ndege utaweza kujitia mashakani ukazuilika safari. |
| Nguo za fakhari, vipodozi vya wanawake n.k. | Haifai kabisa kuchukua kwani unatakiwa ujiepushe na kila linalochukiza ili usalimike na 'ibaadah zako. |